Dondoo ya Sera 1:2016

Maelezo ya Ripoti ya Mbeki Kuhusu Uhamishaji Haramu wa Fedha kutoka Barani Afrika

Ni kwa Jinsi Gani Tanzania Inapaswa Kukabiliana na Uhamishaji Haramu wa Fedha

Februari 2015 Jopo la Ngazi ya Juu Kuhusu Uhamishaji Haramu wa Fedha kutoka Barani Afrika, likiongozwa na Mwenyekiti wake Rais Thabo Mbeki, liliwasilisha ripoti yake kwa Tume ya Umoja wa Afrika/Tume ya Umoja wa Kimataifa ya Kiuchumi Barani Afrika (AUC/ECA). Ripoti ilionesha kuwa nchi za Kiafrika hupoteza kwa wastani dola bilioni 50 kwa mwaka kutokana na uhamishaji haramu wa fedha. Shughuli za kibiashara za sekta binafsi ndizo zinazochangia kwa kiwango kikubwa uhamishaji haramu wa fedha (IFFs), zikifuatiliwa na uhalifu uliopangwa, kisha shughuli za sekta ya umma. Vitendo vya rushwa vinachukua nafasi kubwa katika kuwezesha uhamishaji huu. Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Makampuni ya Kimataifa huhamisha faida kwa makampuni tanzu yenye kodi ndogo au mamlaka za kisiri ambapo mara nyingi hayo makampuni tanzu ni makampuni hewa, mengi yakiwa na mwajiriwa mmoja au wawili tu, wakati shughuli zilizo nyingi hufanyika katika nchi nyingine.

Tamko hili linawasilisha mambo muhimu yaliyofichuliwa na ripoti hiyo na mapendekezo kwa Serikali za Kiafrika – ikiwemo Tanzania.

Matokeo Muhimu

- ✓ *Uhamishaji haramu wa fedha kutoka barani Afrika ni mkubwa na unaongezeka.*
- ✓ *Kukomesha uhamishaji haramu wa fedha ni suala la kisiasa*
- ✓ *Uwazi ni muhimu katika masuala yote yanayohusu uhamishaji haramu*
- ✓ *Njia za kibiashara za uhamishaji haramu wa fedha zinahitaji ufuatiliaji wa karibu zaidi*
- ✓ *Utegemezi wa nchi za Kiafrika kwa uziduaji wa mali asili kunazifanya kuwa katika mazingira yanayorahisisha uhamishaji haramu wa fedha*
- ✓ *Ubunifu wa mbinu mpya zinazopelekea katika uhamishaji haramu wa fedha zinajitokeza*
- ✓ *Motisha za kodi kwa kawaida haziongozwi na uchambuzi wa gharama na faida.*
- ✓ *Rushwa na matumizi mabaya ya madaraka yaliyokabidhiwa yanabaki kuwa matatizo endelevu*
- ✓ *Juhudi mpya za ziada zinahitajika katika kukomboa mali na kuzirejesha*
- ✓ *Utakatishaji fedha unaendelea kuhitaji kutazamwa kwa umakini mkubwa*
- ✓ *Uwezo mdogo wa kitaifa na wa kikanda ni kikwazo katika juhudi za kupunguza uhamishaji haramu wa fedha*
- ✓ *Mfumo wa kimataifa usiokamilika wa kukabiliana na uhamishaji haramu wa fedha*
- ✓ *Mamlaka za sheria za siri kuhusu fedha lazima zipitiwe kwa umakini zaidi*
- ✓ *Wadau wa maendeleo wanajukumu kubwa katika kupunguza uhamishaji haramu wa fedha kutoka Afrika.*
- ✓ *Masuala ya uhamishaji haramu wa fedha sharti yaingizwe na kuratibiwa vizuri zaidi katika taratibu na mifumo yote ya Umoja wa Kimataifa.*

Mapendekezo kwa Serikali ya Tanzania

1. **Kabiliana na bei za kibiashara zisizo sawa:** Nchi za Kiafrika zihakikishe kuwa zina sheria na kanuni zinazotamka waziwazi kwamba ni kinyume cha sheria kutamka kwa makusudi bei, kiasi, kiwango cha ubora au kipengele kingine chochote cha biashara ya bidhaa na huduma isiyo sawa au isiyo sahihi ili kuhamisha mtaji au faida kwenye mamlaka nyingine au kudanganya, kukwepa, kuepuka kodi ya aina yoyote ikiwa ni pamoja na ushuru wa forodha na tozo.

Hatua zinazohitajika:

- ✓ *Hakikisha kwamba makampuni yote, makubwa na madogo, yamesajiliwa kwa ajili ya kodi;*
- ✓ *Kanzu data za ofisi za usajili wa makampuni sharti zioanishwe na zile za mamlaka ya kodi.*
- ✓ *Mamlaka za forodha sharti zitumie kanzu data zilizopo kuhusu bei linganifu za bidhaa za biashara kiulimwengu ili kuchambua bidhaa zinazoingia nchini na zinazotoka ili kutambua miamala inayohitaji uhakiki zaidi.*
- ✓ *Anza kukusanya taarifa za miamala za kibiashara na kutengeneza kanzu data kutokana na taarifa hizo, ambazo baada ya hapo zitaweza kutafutwa na kushirikishwa kwa mataifa mengine.*

2. ***Fuatilia uhawilishaji wa bei:*** Ufanisi katika utekelezaji wa kanuni ya uhuru wa wahusika wa pande zote za muamala kila mmoja akijali matakwa yake binafsi unategemea upatikanaji wa data linganifu za bei za bidhaa na huduma

Hatua zinazohitajika:

- ✓ *Hakikisha upatikanaji wa bila gharama na kwa wakati unaotakiwa, wa data zote za bidhaa na huduma katika miamala ya kimataifa kufuatana na mfumo / utaratibu unaokubalika .*
- ✓ *Anzisha vitengo vya uwekaji bei za uhawilishaji haraka iwezekanavyo. Hivi vitengo viwekwe sehemu zinazofaa katika mamlaka za mapato na ziwe na zana zote zinazohitajika kufuatana na uzoefu bora kimataifa.*
- ✓ *Zitake makampuni ya kimataifa kutoa ripoti zinazotosheleza na zinazoonesha taarifa za fedha zilizochanganuliwa ki-nchi.*

3. **Kabiliana na uhamishaji wa faida unaofanywa na makampuni ya kimataifa:** Desturi ambayo kwayo makampuni ya kimataifa huhamisha faida kwa kampuni tanzu zenye kodi ndogo au mamlaka zenye sheria ya usiri ni chanzo kimojawapo kikubwa zaidi ya uhamishaji haramu. Mara nyingi, hizo kampuni tanzu huonekana kwenye maandishi tu, nyingi zikiwa na mfanyakazi mmoja au wawili, wakati shughuli nyingi za kampuni zinafanyika katika nchi nyingine.

Hatua zinazohitajika:

- ✓ *Sharti kuwe na mabadilishano ya moja kwa moja ya taarifa za kodi miongoni mwa nchi za Kiafrika.*
- ✓ *Toa wito kwa mabadilishano ya taarifa zinazohusu kodi kimataifa, chini ya uwezo wa ki-taifa na wa kutunza usiri wa taarifa za biashara ambazo hubadilika kutegemea bei*

4. **Ongeza uwazi:** Uwazi katika umiliki na utoaji uamuzi katika makampuni, ubia, mifuko ya dhamana / amana na taasisi nyingine za kisheria zinazoweza kuwa na mali na kufungua akaunti za benki ni muhimu katika kuweza kutambua ni wapi fedha haramu zinapelekwa na ni nani anayezihamisha.

Hatua zinazohitajika:

- ✓ *Iwe lazima kwa taarifa za mmiliki / mnufaika kuwekwa wazi wakati kampuni zinapoingizwa kisheria (incorporated) au mifuko ya dhamana / amana zinaposajiliwa au wakati wahusika wa pande zote wanapoingia kwenye mkataba na serikali.*

5. **Pitia mikataba ya ulipaji kodi mara mbili (double taxation agreements):** Mikataba ya ulipaji kodi mara mbili inaweza kuwa na vifungu ambavyo vina madhara kwa ukusanyaji wa rasilimali za ndani ya nchi na vinaweza kutumika kurahisisha uhamishaji haramu wa fedha

Hatua zinazohitajika:

- ✓ *Pitia mikataba ya sasa na ijayo, hususan iliyopo yenye mamlaka ambazo zinahusika na uhamishaji haramu wa fedha, kuhakikisha kuwa hazitoi fursa za matumizi mabaya.*
- ✓ *Fikiria / jaribu kutumia modeli ya Mkataba wa Kodi Mara Mbili ulioandaliwa na Jopo la Usimamizi wa Kodi Barani Afrika (African Tax Administration Forum-ATAF).*

6. Zuia "mbio za kwenda chini" kuhusu motisha za kodi:

Hatua zinazohitajika:

- ✓ *Ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC) sharti utumike ili kuweka viwango vya motisha za kodi kuzuia mashindano ya kuvutia uwekezaji wa nje moja kwa moja.*
- ✓ *Jiunge na ATAF (Jopo la usimamizi wa kodi barani Afrika) na kuipa msaada utakaohitajika , ikiwa ni pamoja na msimamo wa kisiasa katika michakato ya kikanda barani Afrika kama vile mikutano ya AU/ECA ya Mawaziri wa Fedha*

7. Kuwa makini sana na sekta ya uziduaji

Hatua zinazohitajika:

- ✓ *Jiunge na mipango ya kujitolea kama vile Mpango wa Uwazi Katika Viwanda vya Uziduaji (EITI).*
- ✓ *Tetea / shawishi kwa utoaji wa taarifa wa lazima kisheria wa nchi kwa nchi na mradi kwa mradi mara moja, katika sekta ya uziduaji na baada ya muda mfupi katika sekta nyingine zote*

8. Imarisha na Anzisha Taasisi Zinazowajibika Kuzuia Uhamishaji Haramu wa Fedha (IFFs)

Hatua zinazohitajika:

- ✓ *Imarisha au anzisha vitengo vya usalama wa fedha, mashirika ya kuzuia ufisadi, mashirika yanayosimamia forodha na mipaka, mashirika ya mapato, mashirika ya kuzuia rushwa na mashirika ya makosa yanayohusiana na fedha.*
- ✓ *Tengeneza njia na mbinu za kushirikishana taarifa na kuratibu shughuli miongoni mwa taasisi na mashirika ya Serikali yenye jukumu la kuzuia uhamishaji haramu wa fedha (IFFs), uratibu huo ukiongozwa na kitengo cha usalama wa fedha cha nchi husika.*
- ✓ *Weka usimamizi wa mabenki na taasisi za fedha zisizo za kibenki chini ya benki kuu na mashirika ya usimamizi wa fedha. Usimamizi huo sharti uwe na utaratibu wa kisheria wa kutaka utoaji wa taarifa za miamala ambazo zinaweza kuwa na tope la shughuli haramu.*

9. Zuia uhamishaji haramu wa fedha kwa njia ya makosa ya jinai: Uwindaji haramu; madawa, zana za vita na biashara haramu ya binadamu; uwizi wa mafuta na madini; na aina nyingine za makosa ya jinai zinazozalisha fedha zinaongeza IFFs, wakati mwingine zikitumia mbinu zile zile za kibiashara zinazotumika kukwepa kodi na ushuru wa forodha kuhamisha fedha zilizopatikana kwa njia hizi za jinai nje ya Afrika.

Hatua zinazohitajika:

- ✓ *Hakikisha kuwa wachunguzi wenye jukumu la kutambua wahalifu wanaoendesha shughuli hizi pia wanahitajika, wanafunzwa na kujengewa uwezo kuchunguza vipengele vya kifedha vya kesi hizi, pia kuendesha mashitaka dhidi ya wale wanaowezesha uhamishaji na utakatishaji wa mwenendo wa makosa haya.*
- ✓ *Shirikishana taarifa na vitengo vingine vya usalama wa fedha barani Afrika kuhusu kesi za watu na makampuni yaliyoshitakiwa kwa kuwezesha uhamishaji na utakatishaji wa mwenendo wa kesi hizi ili shughuli haramu mipakani na jinsi zinavyoendeshwa ziweze kugundulika.*

10. Zuia uhamishaji haramu wa fedha kwa njia ya rushwa: Viwango vya kiulimwengu dhidi ya rushwa na dhidi ya utakatishaji fedha vinataka taasisi za fedha kuchunguza akaunti za baadhi ya watu kwa umakini na ufuatiliaji mkubwa, ikiwa ni pamoja na akaunti za viongozi wakuu serikalini, viongozi wa vyama vya kisiasa, watendaji wa mashirika ya kibiashara yanayomilikiwa na serikali na wengine wenye uwezo wa kufikia mali nyingi za serikali na mamlaka ya kuzielekeza. (mara nyingi wanaitwa watu wanaojulikana kisiasa (politically exposed persons, au PEPs).

Hatua zinazohitajika:

- ✓ *Chapisha idadi ya watu wanaojulikana kisiasa (PEPs), pamoja na taarifa rasmi walizozijaza za mali zao na taarifa za kama sheria za nchi husika zinakataza au zimewekea mipaka finyu uwezo wa PEPs kuwa na akaunti nje ya nchi.*
- ✓ *Kuzitaka taasisi za fedha za nchi za kigeni, kutoa maelezo ya akaunti za PEPs walioko katika orodha yao, ingekuwa vizuri zaidi taarifa hizo zitolewe moja kwa moja kama sehemu ya taratibu za kubadilishana taarifa za fedha.*
- ✓ *Hakikisha kuwa umma unaweza kupata taarifa ya bajeti ya taifa na vitengo vyake, na ya kwamba michakato na taratibu za utengenezaji wa bajeti na ukaguzi ziko wazi kwa umma.*
- ✓ *Tumia mifano ya uzoefu bora katika uandaaji wa mikataba iliyo wazi ili kupunguza IFFs kupitia taratibu za manunuzi ya serikali.*

Mapendekezo yaliyotolewa ni ya lazima lakini si yo masharti yanayotosheleza kwa nchi za Afrika kupambana na IFFs. Inaelekea kuwa mikakati ya ziada inahitajika.

11. Mikakati ya ziada katika kupambana na uhamishaji haramu wa fedha (IFFs) kutoka Afrika

Mikakati inayohitajika katika ngazi za taifa na za kikanda:

- ✓ *Nchi za kiafrika zipitishe chombo cha kanuni katika mfumo wa azimio kuhakikisha mapambano dhidi ya IFFs na kuhimiza hatua kama hizo katika ngazi ya kimataifa*
- ✓ *Kutokana na jukumu muhimu la asasi za kiraia (vyombo vya habari, asasi zisizo za kiserikali, wasomi na wanoa bongo) katika juhudi za kupunguza IFFs, ni muhimu wapewe nafasi na uhuru wa kisheria unaohitajika kwa ajili ya utetezi, uanaharakati na utafiti katika eneo hili.*
- ✓ *Ingiza IFFs katika kifungu cha 22 cha Mkataba wa Umoja wa Kiafrika Kuhusu Kuzuia na Kupambana na Rushwa.*
- ✓ *Utaratibu wa Mapitio Rika (The African Peer Review Mechanism) uingize masuala ya IFFs katika hojaji zao za mapitio ya ki-nchi.*
- ✓ *Fanya utafiti wa mbinu na mabadiliko yaliyoko ulimwenguni na kikanda na katika nchi binafsi za kiafrika kuwezesha utoaji kodi kwa makampuni makubwa ya kimataifa kufuatana na mahali shughuli zao za kiuchumi zinapoendeshwa, kwa kuweka maanani viwango vya sasa vya kimataifa na fursa za kuboresha hivyo viwango*
- ✓ *Toa mamlaka kwa ECA kufanya utafiti kuhusu uchambuzi wa gharama na faida za motisha za kodi ili kusaidia kutoa mwongozo kwa nchi za Kiafrika katika kuandaa mifumo kama hiyo yenye nia ya kuvutia uwekezaji wa kigeni wa moja kwa moja.*
- ✓ *Nchi za kiafrika zifikirie kuratibu juhudi na kuwasilisha nafasi zao katika umoja wa kikanda au umoja mkubwa zaidi katika majadiliano na mikutano ya OECD. Pale ambapo hatua zinachukuliwa na OECD na nchi za kiafrika zinaona kwamba hatua hizo zitaumiza nchi zao au bara lote kwa ujumla, nchi za kiafrika zipendekeze na kuchapisha hatua ambazo nchi za kiafrika zinaweza kuchukua ili kukabiliana na vitendo vya uhamishaji wa faida ambavyo vina madhara kwa nchi za kiafrika.*

Policy Forum
S.L.P 38486, Dar es Salaam
Simu: +255 22 2780200/255 782317434
Barua pepe: info@policyforum.or.tz | Tovuti: www.policyforum.or.tz

The Inter-Faith Standing Committee for Economic Justice & Integrity of Creation